**HOTUBA YA KATIBU MKUU KIONGOZI YA UFUNGUZI WA MKUTANO WA FARAGHA WA MAKATIBU WAKUU, MAKATIBU TAWALA WA MIKOA NA NAIBU MAKATIBU WAKUU UTAKAOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA JAKAYA KIKWETE, IKULU DAR ES SALAAM, TAREHE 13 - 14 JULAI, 2022**

---

***Mha. Zena A. Said, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar,***

***Makatibu Wakuu,***

***Makatibu Tawala wa Mikoa,***

***Naibu Makatibu Wakuu,***

***Wakuu wa Taasisi,***

***Watoa Mada,***

***Wageni Waalikwa,***

***Mabibi na Mabwana.***

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…. Kazi Iendelee…!

Awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya Mkutano huu wa Faragha wa Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Naibu Makatibu Wakuu.

Pia, nawashukuru wote kwa kuitikia wito wa kuhudhuria Mkutano huu muhimu ambao ni wa kwanza tangu Serikali ya Awamu ya Sita ilipoingia madarakani. Lakini pia, ni mara yangu ya kwanza kukutana nanyi katika Mkutano wa aina hii tangu nilipoteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kushika nafasi ya Katibu Mkuu Kiongozi. Karibuni sana Washiriki wote katika Mkutano huu.

Kipekee, napenda kumshukuru Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kukubali wito wangu na kutenga muda wake kwa ajili ya kujumuika nasi katika Mkutano huu.

***Ndugu Washiriki***;

Mkutano huu ni wa kikanuni kwa kuwa unafanyika kwa mujibu wa matakwa ya ***Mwongozo wa Mikutano ya Makatibu Wakuu wa Mwaka 2008, Toleo la 2016.*** Mwongozo huo unaelekeza kuwa Mkutano huu kufanyika kwa lengo la kujadili taratibu na mbinu zinazounganisha utendaji kazi kati ya Serikali Kuu; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Watendaji Wakuu wa Wizara na Mikoa. Kwa muktadha huo, Mkutano huu unasaidia: -

***(i) Kubadilishana maarifa na uzoefu;***

***(ii) Kufahamiana na kujenga ushirikiano na mahusiano ya kikazi katika utekelezaji wa shughuli za Serikali;***

***(iii) Kupeana taarifa katika masuala mbalimbali ya kisera na kiutendaji;***

***(iv) Kujadili changamoto zilizopo za kitaalam na kitaasisi katika utekelezaji wa sera, mipango na program za Serikali na kutafuta mwelekeo sahihi wa utekelezaji wake; na***

***(v) Kukumbushana wajibu katika utekelezaji wa majukumu yetu kama Viongozi, Wasimamizi, Watendaji Wakuu na Watumishi wa Umma.***

***Ndugu Washiriki***;

Kama mnavyofahamu, Serikali ipo katika maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ambayo itafanyika tarehe 23 Agosti, 2022. Sensa hiyo ina umuhimu mkubwa kwa kuwa itasaidia kupatikana kwa takwimu sahihi na taarifa za msingi za hali ya kidemografia, kijamii na kiuchumi kuhusu watu na makazi.  Takwimu na Taarifa hizo zitaiwezesha Serikali kubuni, kupanga na kutekeleza kisayansi mipango ya uchumi na maendeleo ya Nchi kwa ujumla.

Kutokana na umuhimu wa Sensa, Mkutano huu umebeba kauli mbiu ya ***"Sensa ya Watu na Makazi kwa Maendeleo ya Taifa".*** Hali hii imezingatia wajibu mlio nao kama watendaji na wasimamizi wakuu wa shughuli za Serikali ngazi ya Wizara na Mikoa katika kufanikisha suala hili nyeti na lenye maslahi mapana kwa Taifa. Tutapata mada mahsusi kuhusu suala hili itakayotolewa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

***Ndugu Washiriki***; pamoja na Mada kuhusu Hali ya Maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, mada nyingine zitakazowasilishwa katika Mkutano huu ni: -

***(i)*** ***Taratibu za utendaji wa kazi Serikalini;***

***(ii)*** ***Mifumo ya Ukaguzi na Udhibiti wa Ndani kwa Matumizi ya Raslimali za Serikali;***

***(iii)*** ***Uwajibikaji na Usimamizi Katika Matumizi ya Rasilimali za Taifa;***

***(iv)*** ***Maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo baada ya kufikia ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025;***

(v) ***Mfumo wa Ubunifu, Upangaji, Uratibu, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Shughuli za Mashirika/Taasisi za Umma katika Ulimwengu wa Kibiashara (Corporate World) kwa kuzingatia Dira na Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa; na***

(vi) ***Tathmini na Mapendekezo ya Kuboresha Mfumo wa Kubuni, Kupanga, Kuratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Serikali.***

***Ndugu Washiriki***;

Wakati naapishwa kushika nafasi ya Katibu Mkuu Kiongozi, nilieleza umuhimu na uhitaji wa kuimarisha usimamizi na uratibu wa shughuli za Serikali kutokana na muundo wa Serikali ulivyo. Kwa sasa, zipo Ofisi/Wizara 24; Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali 347; Mikoa 26 na Wilaya 139 kwa Tanzania Bara; na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184, ikijumuisha Halmashauri za Majiji 6, Manispaa 20, Miji 21 na Wilaya 137.

Kwa muundo huu wa Serikali, ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Serikali na kufikia matarajio na matamanio ya wananchi, ni lazima tuwe na mfumo thabiti wa upangaji, uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Serikali. Tusipokuwa na mfumo huo, utekelezaji wa shughuli za Serikali utaendelea kudorora, hivyo ni lazima tuchukue hatua. Hali hiyo, ndiyo ilinisukuma kuunda Timu kwa ajili ya kufanya tathmini na kupendekeza hatua za kuboresha mfumo huo. Tutapata nafasi ya kujadili Taarifa ya Tathmini iliyoandaliwa na Timu hiyo kama nilivyobainisha hapo awali. Ni matarajio yangu kuwa, Mkutano huu utakuwa ni chachu ya kupata maoni, ushauri na mawazo ya namna ya kuboresha mfumo huo.

*Ndugu Washiriki*;

Serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo; huduma za jamii, ikiwemo elimu, maji na afya; na miradi ya maendeleo katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, kaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zinazofanyika kila mwaka zinabaini kuwepo kwa upungufu katika usimamizi wa miradi, na shughuli nyingine za Serikali ikiwemo ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo, pamoja na vitendo vya wizi na ubadhilifu wa mali za umma.

Kimsingi, ukiukwaji huo pamoja na vitendo vya ubadhilifu na wizi wa mali za umma na uzembe wa aina yoyote ile katika usimamizi wa miradi ya maendeleo havikubaliki. Ninyi kama Maafisa Masuuli mnalo jukumu la kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali za umma na mnalazimika kulitekeleza jukumu hilo kwa bidii na nguvu zote, ili kuhakikisha fedha zinazotolewa kwa ajili ya miradi hiyo zinatumika kama ilivyopangwa, na hivyo kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kwa muktadha huo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali tupo nao hapa leo kwa ajili ya kujadili masuala haya ili tuweze kuwa na mifumo thabiti ya usimamizi na udhibiti wa matumizi ya rasilimali za umma.

Kwa ujumla, mada zote zitakazojadiliwa katika Mkutano zinalenga kuongeza ubunifu, tija na ufanisi katika mifumo ya utendaji Serikalini. Hivyo, tuutumie Mkutano huu vyema kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja katika maeneo mbalimbali. Maoni, ushauri na mapendekezo

mtakayotoa ni muhimu kwani yatasaidia kuboresha baadhi ya taratibu na mifumo ya utendaji Serikalini.

***Ndugu Washiriki***;

Vile vile, pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kitaifa, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuimarisha na kufufua uchumi kutokana na athari za Ugonjwa wa UVIKO – 19 na vita vya Urusi na Ukraine. Hatua hizo ni pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya sekta za uzalishaji; kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuvutia mitaji na uwekezaji; na kuimarisha sekta ya utalii. Hatua hizi haziwezi kufanikiwa endapo ninyi kama watendaji wakuu wa Serikali katika Wizara na Mikoa hamtakuwa na utayari, weledi, ubunifu na uthubutu wa kusimamia utekelezaji wake. Hivyo, tutimize wajibu wetu ipasavyo ili kufanikisha jitihada hizo za Serikali.

Baada ya kusema haya, napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru tena wote kwa kuja kushiriki katika Mkutano huu muhimu kwa utendaji wa kazi zetu za kila siku za usimamizi na utekelezaji wa shughuli za Serikali kwenye maeneo yetu.

Hivyo, sasa natamka rasmi kwamba, Mkutano huu wa Faragha wa Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Naibu Makatibu Wakuu wa Mwaka 2022 umefunguliwa rasmi.

***ASANTENI KWA KUNISIKILIZA!***

*********************************************